TANGAZO LA SERIKALI NA. 225 la tarehe 24/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA 355)

______

**AMRI**

______

*(Imetolewa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

______

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA MASAWI YA MWAKA, 2023.

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Masawi ya mwaka, 2023

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura (355)

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji)kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Mpango wa Urasimishaji lipo ndani ya Mipaka ifuatavyo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ML1 yenye majira - nukta 803471MS, 9497184KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini -Mashariki katika uelekeo wa KZ80$^0$44'11''MS kwa umbali wa kilomita 0.806 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ML2 yenye majira - nukta 804250MS, 9496977KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa kufuata barabara Arusha – Kondoa katika uelekeo wa KS10$^0$42'10"kwa umbali wa kilomita0.937 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ML3 yenye majira - nukta 804203, 9496041; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini- Masharikikwa kufuata barabara Arusha – Kondoa katika uelekeo wa KS10$^0$42'10"kwa umbali wa kilomita0.937 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ML4katika uelekeo wa KS09$^0$32'15"MS kwa umbali wa kilomita0.375 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ML5 yenye majira - nukta 804265MS, 9495671KZ; baada ya hapo mpaka unaelekeaKusini - Magharibi katika uelekeo wa KS45$^0$15'55''MGkwa umbali wa kilomita 0.614 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ML6 yenye majira - nukta 803764, 9495428; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS20$^0$10'37''MG kwa umbali wa kilomita 1.414 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6 Februari, 2023

BANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*